



Don alikuwa nyani
mkubwa.


Alikuwa mchokozi.




Don ndiye alikuwa
chifu wa nyani wengine.




Wafuasi wake walimpatia
kitambaa maalum.



"Nitakivaa kichwani,"
Don alisema.




"Kila mmoja afuate
masharti yangu. Msinihoji!"
Don alipiga kelele.




Wafuasi
walimfuata chifu wao.

Don iliporuka, kila
mmoja aliruka.




Lakini, kile kitambaa,
kilimkaza sana.




Don aligusa kichwa
alikoumia.

Nyani pia waligusa
vichwa vyao.




"Hapa panuma,"
Don alisema.

Nyani pia walisema,
"Hapa panauma."




Alisema, "Hii
imekazika sana!"

Wao pia walisema,
"Hii imekazika sana."



Don alianguka
kutoka juu.

Wote walimuiga
wakaanguka.



Nyani aliyekuwa
chifu alikufa.

Wafuasi wake
waliumia, lakini waliishi.